UJUMBE WA KERO ZA DIASPORA KWA SERIKALI YA TANZANIA ILI KURAHISISHA USHIRIKI WA DIASPORA KATIKA UWEKEZAJI NA UJENZI WA UCHUMI WA NCHI.

Kwa muda mrefu Vyama na Jumuiya za Watanzania waishio nje ya nchi(Tanzania) vimekuwa vikiwakilisha kero mbalimbali kwa serikali Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Kuiomba kuweka mazingira bora ya Kisheria ili kuondoa wasiwasi na kurahisisha uwekezaji kwa Diaspora. Uwekezaji mkubwa wa kibiashara,Viwanda na uwekezaji wa kibinafsi kwa Diaspora mmoja mmoja.

Kero kadhaa ziliwakilishwa ili kutafuta njia nzuri ambayo haitahatarisha usalama wa nchi, lakini itakayowezesha kuwa na sheria rafiki za uwekezaji kwa Diaspora wote. Moja ya mapendekezo hayo ni kwa Diaspora kujikusanya na kuanzisha chombo kimoja cha diaspora kitakachokuwa kiunganishi kati ya Serikali na Diaspora.

Kwa sasa hilo limefanyika ambapo Diaspora imeanzisha baraza la diaspora la watanzania duniani linalojulikana kama **Tanzania Global Diaspora Council-TDC Global**. Lililosajiliwa rasmi nchini Sweden **18.05.2018**. Baada ya usajili wa **TDC Global**, tumeona serikali ikishirikiana na kutekeleza kwa kasi ya ajabu mambo muhimu yaliyokuwa yakiombwa na Diaspora kwa muda mrefu.

Mojawapo ikiwemo kuanza kwa mchakato wa kuandaliwa kwa sera rasmi ya Diaspora ya Tanzania, itakayokuwa njia ya kuelekea kwenye mabadiliko ya sheria zitakazorahisha na kujenga uaminifu kati ya Diaspora na serikali.

Pamoja na nia nzuri ya serikali kutafuta ufumbuzi wa vikwazo hivyo ni vyema sisi kama Diaspora tuviweke wazi zaidi ili serikali iweze kuzitambua vizuri kero hizo na kujipanga vizuri kuzitafutia ufumbuzi wa kudumu kwa zile zinazowezekana na kutolea ufafanuzi mzuri kwa zile zinazotakiwa kupewa muda zaidi wa majadiliano na utekelezaji

Baraza la Diaspora la Tanzania duniani linaomba kuwakilisha kero na faida zitakazopatikana na pande zote mbili pale kero hizo zitakapo ondolewa kama ifuatavyo:

1.**Kutokuwepo kwa Uraia Pacha**:

Uraia pacha ni ombi la muda mrefu la Diaspora wote kwa Serikali ya Tanzania. Sheria itakapobadilishwa na kuruhusu Uraia pacha, hakutakuwa na haja ya Diaspora kuwa na ombi jingine lolote la kubadilisha sheria au kutunga sheria mpya ya kupewa upendeleo maalum kwa Diaspora kuweza kushiriki katika ujenzi wa taifa.

Ombi pekee litakalokuja hapa ni kuwaruhusu kisheria Diaspora wote waliokuwa na uraia wa Tanzania, lakini kwa sasa wana uraia mwingine watambulike kuwa uraia wao wa awali wa Tanzania umerudishwa kwao rasmi kisheria.

Kero hii ya kutokuwa na uraia pacha ni kikwazo kikubwa na kitu kinachoijengea hofu sana jamii yote ya Diaspora, Kuanzia katika eneo la Urithi wa mali za wazazi/familia za Diaspora zinaishi Tanzania hadi uwekezaji kwa Diaspora wenyewe nyumbani Tanzania. Lazima tukabali kuwa uwekezaji wowote ule ni lazima unufaishe pande zote mbili. Yule anayewekeza na kwa wale/Nchi anayowekeza wanufaike kisheria bila ya upande mmoja kuwa na hofu ya kuwepo uwezekano wa kupoteza mali walizowekeza.

2. **Malipo ya Viza Kwa Diaspora na Wenza wao**:

Diaspora wengi wamepunguza idadi ya watu wanaowategemea kusafiri nao pale wanapokuja Tanzania, kutokana na malipo ya Visa wanazotakiwa kuwalipia. Malipo ya Viza huwa kikwazo kwa kuwa ni kitu cha lazima kwa kila Diaspora mwenye uraia mwingine. Hii hulazimika Diaspora wengi kupanga ni nani ataongozana nae katika familia yake. Kupunguza idadi ya watu wanaoongozana nao kunapunguza matumizi ya kawaida ambayo yangefanywa na watu hao wakati wa wakiwa Tanzania.
Pesa ambazo zingekuza vipato vya watanzania wanaouza chakula, vinywaji na nyumba za kupanga za kuwahifadhi Diaspora hao. Pesa zote hizi pia zingeongeza pato la serikali kupita kodi zilizomo kwenye malipo hayo.

3. **Malipo tofauti katika vyombo vya Usafiri na Zanzibar.**

Kumekuwa na utaratibu ambao Diaspora wasio na uraia wa Tanzania ulazimika kulipa nauli kubwa kwa usafiri kati ya Zanzibar na Bara. Hii imewafanya wengi kujisikia kubaguliwa, na hivyo kuacha kusafiri kwenda Zanzibar au Bara katika safari zao wakiwa Tanzania. Ikumbukwe kwamba kila unapoweka gharama zisizo za lazima watu hawa huwasimulia wenzao na kusambaza ujumbe ambao unachangia kupungua kwa idadi ya Diaspora wanaosafiri kutoka upande mmoja wa muungano kwenda upande mwingine. Kwa kufanya hivyo serikali inapoteza pesa nyingi ambazo zingetokana na kodi za matumizi ya Diaspora hao.

4. **Ubadilishaji wa pasi za kusafiria kwa wale wenye uraia**

Kubadilisha Passport kumesababisha Diaspora wengi kuingia gharama kubwa, kwa kusafiri na kufanya malipo mengine ya ziada ili kukamilisha zoezi hilo.Vitu vinavyotakiwa kuwakilishwa kwa kupata passport mpya ya kielektroniki umekuwa ni

changamoto kubwa kwa wana Diaspora.Tunaomba serikali ijitahidi kuweka vyombo vya kukusanya taarifa muhimu katika Balozi zetu Duniani pote palipo na ofisi zetu.

5. **Diaspora kutoshirikishwa kuchagua viongozi katika uchaguzi**

Diaspora wengi wameomba uwezekano wa kuwekwa utaratibu ili waweze kuchangua viongozi katika uchaguzi mkuu. Kwa sasa hakuna utaratibu uliowekwa na Serikali kuwawezesha wao kupiga kura wakiwa katika nchi zao za makazi. Mapendekezo yao ni kuwa utaratibu uwekwe ili waweze kupiga kura katika uchaguzi wa Rais katika ubalozi na uchaguzi wa wabunge na madiwani kutoka wilaya zao za makazi walizokuwa wanaishi hadi walipoondoka nchini.

6. **Kuondolewa Viza kwa wenza wa Diaspora wenye uraia wa Tanzania**.

Maombi yao ni kuwa Diaspora mwenye uraia anapokuja Tanzania na mke au mume basi aruhusiwe kukaa kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kuhitaji kuongeza viza au kuondoka na kurudi nchini na ikiwezekana kupitia mwenza wake basi asilipishwe viza hata wakati wa kuingia nchini.

7. **Kuchelewa kulipwa kwa wanafunzi wanaosomeshwa na serikali**

Wanafunzi wengi wanaomba malipo ya posho zao na mikopo isicheleweshwa sana. Wanaomba pia wapatiwe kitengo maalum kuharakishiwa malipo yao.

8. **Kutotambuliwa kwa watu wenye ujuzi kama ni rasilimali**

Diaspora wengi wenye ujuzi wameomba serikali iweke utaratibu rasmi wa kuwatambua ili waweze kutumiwa vizuri pale wanapofaa kulingana na ujuzi wao kabla ya kutumia wageni.

9. **Kutokuwepo kwa sheria maalum ya kuwapendelea Diaspora wazawa**.

Diaspora wengi wameiomba serikali itunge sheria maalum itayowapa upendeleo Diaspora wazawa waliobadilisha uraia wao ili waweze kunufaika na baadhi ya mambo kutokana na asili yao. Wanaomba Serikali itunge sheria itayowapa haki katika mambo yafuatayo:

a. Kumiliki aridhi kama watanzania wengine.
b. Kuingia nchini Tanzania na kukaa muda wowote bila kuhitaji viza.
c. Wake na waume zao kuruhusiwa kuwa na haki sawa ya kuingia na kuishi Tanzania bila ya kuhitaji visa kama Diaspora wenyewe bila kujali urai wao.
d. Watoto wa Diaspora hawa warusiwe kurithi mali za wazazi wao hata kama wao watakuwa na uraia mwingine.
e. Diaspora waliobadili uraia waruhusiwe kurithi mali za wazazi, na jamaa zao nchini Tanzania kama Watanzania wengine.

f. Kuwa na haki ya kuanzisha biashara na viwanda kama watanzania wengine bila kuhitaji kupitia TIC.
g. Diaspora kupitia sheria hii wanaomba pia wawe na haki ya kuchagua na kuchaguliwa katika uchaguzi wa ngazi za chini kama udiwani na ujumbe wa nyumba kumi.
h. Waruhusiwe kuchaguliwa katika vyeo vya kuteuliwa kama vile ukuu wa wilaya na mikoa kama mwenye mamlaka ya uteuzi ataona wanafaa kwenye nafasi hizo.
i. Warusiwe kupatiwa vitambulisho vya taifa vitakavyoonyesha kuwa wao ni raia wa nchi nyingine lakini asili yao ni Tanzania. Kupitia vitambulisho hivi wataweza kujitambulisha katika maeneo mbalimbali bila usumbufu wowote watakapokuwa Tanzania na vitambulisho hivi vitatumika kuwatambua wakati wanaingia Tanzania.

Yapo mengi yanayosemwa katika kero hii ya kutokuwa na sheria maalumu ya upendeleo kwa Diaspora waliobadilisha uraia wao. Lakini haya ndio yaliyorudiwa sana. Tutaendelea kuwakilisha mengine katika vikao vijavyo na serikali. Kama tutaruhusiwa kufanya hivyo.

Mwisho ninaomba niziorodheshe kero tu bila kuzitolea maelezo:

1. Kutokuwepo kwa sheria ya upendeleo maalumu kwa Diaspora wazawa waliobadili uraia.
2. Uraia pacha
3. Kulazimishwa kutoka nje ya nchi pale Diaspora anapotaka kuongeza viza baada ya siku 90 za viza ya kawaida kwisha.
hizo 90 nchini Tanzania.
4. Diaspora kulazimika kutafuta vibali vya uwekezaji kabla ya kufanya uwekezaji.
5. Gharama za tozo katika kutembelea mbuga za wanyama.
6. Kutokuwepo utaratibu mzuri wa kupatiwa mikopo Diaspora kwa dhamana ya kazi wanazofanya ughaibuni.
7. Watanzania wanaotaka kuja huku kusoma(ambao sasa ni diaspora) wanasema wanalazimika kutafuta barua za mialiko ili wapatiwe pasi wakati pasi ni haki yao. Wanaomba kigezo cha kulazimishwa kuleta barua ya mualiko kiondolewe.
8. Vitambulisho vya Taifa vitolewe na ubalozi ili kupunguza ghalama kwa Diaspora.

Kwa niaba ya baraza letu nashukuru sana serikali kutupatia nafasi hii hata ya kutusikiliza tu. Tumefarijika sana na Mungu awabariki sana.

Norman Jasson

Norman Jasson
Mwenyekiti
TDC Global.

PAMOJA TWAWEZA
MTU KWAO NDIO NGAO